Dk. Mlanzi, alisema ... wanamipango, hufanyika kila mwaka kwa lengo la kubadilishana uwezo na mada mbalimbali zitawasilishwa."

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais ... Naibu Waziri wake, Deogratius Ndejembi, kabla ya kufungua mkutano ... Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mkoani Manyara, jana.

UHURU UK 6.

# *Ufugaji mifugo kienyeji chanzo kushuka soko nyama kimataifa*

**Na WARIOBA IGOMBE**, *Morogoro*

UFUGAJI wa kienyeji wa mifugo mbalimbali nchini, umetajwa kuwa chanzo cha kushuka soko la nyama kimataifa ambapo wametakiwa kijikita zaidi katika ufugaji wa kisasa na kuongeza tija.

Hayo yalisema juzi na Ofisa Mifugo Mwandamizi kutoka Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Martin Mkindi, wakati akitoa elimu ya umuhimu wa unenepeshaji mifugo kwa wafugaji na wafanyabiashara wa nyama wilayani Mvomero, mkoani Morogoro.

Mkindi alisema kwamba, wafugaji wengi wamekuwa wanafuga kienyeji bila kuzingatia kanuni bora za ufugaji, hali inayosababisha uzalishaji wa mifugo nchini, kuwa chini ya kiwango kinachohitajika katika soko zima la kimataifa.

"Nyama zinazotoka nchini, zimeonekana kutokuwa bora kwa kiwango cha soko la kimataifa, hii inatokana na wafugaji wengi kuendesha shughuli zao hizo za kienyeji, hali inayowafanya ufugaji wao usiwe na tija kwa Taifa," alisema.

Ofisa huyo, aliwataka wafugaji kujikita zaidi katika unenepeshaji mifugo na kuongeza thamani ya nyama, kwani kutasaidia kuwa na ushindani katika soko la kimataifa kwa kuzingatia kanuni na utaratibu wa unenepeshaji mifugo.

Alisema kitendo cha wafugaji kufuga kisasa na kuondokana na tabia ua kufuga kienyeji, kutasaidia kukuza uchumi unaotokana na sekta ya mifugo nchini, kwani wafugaji watakuwa na uhakika wa soko la nyama jambo ambalo lina manufaa kwa Taifa.

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dk. Daniel Mushi, alisema soko la kimataifa kwa siku, linahitaji ng'ombe 5,635 zinazokidhi viwango vya kimataifa, mbuzi na kondoo 13,900 kukidhi hitaji la kusafirisha nyama au mifugo mara moja nje ya nchi.

Dk. Mushi alisema changamoto ya upatikanaji mifugo hiyo kutokana na wafugaji na baadhi ya wafanyabiashara kufuga kienyeji bila kuzingatia faida, zinapatikana katika ufugaji huo wa kisasa.

Alisema soko la kimataifa, halizingatii wingi wa mifugo isipokuwa hujikita zaidi katika mifugo bora na kuzalisha nyama inayokidhi viwango vya kuuzwa nje ya nchi.

"Viwanda vingi vya nyama vinazalisha zaidi nyama ya mbuzi na kondoo kuliko ya ng'ombe, kwa sababu ya ukosefu wa ng'ombe bora, hii inasababishwa na ufugaji wa kizamani ambao unazingatia idadi kubwa ya mifugo bila kujali ubora wake," alisema.

Nao, wafugaji na wafanyabiashara wa nyama akiwemo Ramadhani Chandira, alitaja moja ya changamoto inayowakwamisha katika ufugaji wa kisasa ni hali duni ya maisha.

Emmanuel John, yeye alisema ukosefu wa elimu ya ufugaji wa kisasa ni kikwazo kwa baadhi ya wafugaji hususan wanaoishi vijijini, akaiomba serikali kupitia Bodi ya Nyama Tanzania, kwenda huko kwa lengo la kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa vijijini.

**MIFUGO**

**NYAMA**

Alisema kwamba, wafugaji wengi wamekuwa wanafuga kienyeji bila kuzingatia kanuni bora za ufugaji, hali inayosababisha uzalishaji...

OPERESHENI OKOA RUAHA

# Ng'ombe 708 wapigwa mnada

## Ni baada ya kukaidi agizo la Serikali Ihefu

IHEFU

NA MWANDISHI WETU

Kama ilidhaniwa kuwa amri au maelekezo yaliyotolewa na mawaziri wa kisekta kuhusu kufutwa kwa makumi ya vijiji na vitongoji ndani ya Bonde la Usangu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni utani, sasa hali imebadilika.

Mwishoni mwa Oktoba mwaka huu, mawaziri hao wakiongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, walizungumza na wananchi wa Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya na kuelekeza kuondoka mara moja kwa wafugaji na wakulima waliovamia eneo la hifadhi.

Maelekezo hayo yalitajwa kuwa ni mapendekezo ya Baraza la Mawaziri ambalo Mwenyekiti wake ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali, timu ya mawaziri na waandishi wa habari wakiongozwa na mwenyeji wao, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Komredi Juma Homera, walitembelea vijiji kadhaa na kushuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa hasa na wingi wa mifugo.

Uvamizi wa wakulima na wafugaji kando ya Mto Ruaha Mkuu na eneo oevu la Ihefu umesababisha mto huo muhimu kwa maendeleo na uchumi wa taifa kushindwa kutiririsha hata tone moja la maji.

"Sisi tunaondoka. Kazi inabaki kwa Komredi Homera. Jipange na timu yako kuhakikisha eneo hili linabaki salama na mazingira yanalindwa," anasema Dk. Angeline kabla ya kupanda helikopta ya jeshi na kuondoka Mbarali. Hiyo ilikuwa Oktoba mwaka huu.

Baada ya kuondoka ugeni huo, Komredi Homera akaliambia JAMHURI kuwa wapo tayari kutekeleza maelekezo ya Rais na Baraza la Mawaziri bila hofu, na kwamba iwapo wangepata uwezeshaji walikuwa tayari hata kuanza kazi siku ile ile!

**Mamia ya ng'ombe wakamatwa, yapigwa mnada**

Mwezi mmoja baadaye, JAMHURI limemtafuta Komredi Homera kutaka kujua hali ikoje Ihefu, naye akajibu: "Agizo la Rais kupitia kwa Dk. Angeline hatujalipuuza. Tunalifanyia kazi na hivi ninavyokuambia, mimi na timu yangu tupo Ihefu."

Homera anasema kuna watu wanaijaribu serikali kwa kupuuza maagizo inayoyatoa, suala ambalo yeye hayupo tayari kuona likiachwa liendelee.

Kwamba hata baada ya kufutwa kwa vijiji na vitongoji na kuwaomba wananchi kuacha kuingia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuvuruga ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu, wapo baadhi yao wameamua kwa makusudi kukaidi.

"Sasa hawa ni wakorofi. Lazima kuwashughulikia. Tumekamata majangili wa tembo ndani ya hifadhi, na pia tumekamata mamia ya mifugo ikiwamo maeneo yaliyopigwa marufuku pembezoni mwa Ihefu," Komredi Homera ameliambia JAMHURI wiki iliyopita.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Baadaye, anamuunganisha mwandishi na mmoja wa maofisa aliokuwa nao kwenye 'Operesheni Okoa Ruaha' aliyemtambulisha kwa jina moja, Siraji, ili kupata 'data' kamili.

Siraji anasema kati ya Novemba 18 na Desemba 3, mwaka huu, jumla ya ng'ombe 708 mali ya wafugaji wakorofi wamekamatwa maeneo ya Ihefu na kupigwa mnada.

"Kwanza, Novemba 18 tulipiga mnada ng'ombe 435, kisha tukauza wengine 172, halafu baadaye ng'ombe 93 na jana (Ijumaa, Desemba 2, mwaka huu) tumewapiga mnada ng'ombe 10," anasema Siraji.

**'Vimemo', vitisho vya wakubwa**

JAMHURI linafahamu kwamba kukamatwa kwa ng'ombe hao kulizua tafrani katika maeneo mbalimbali nchini, na kusababisha Komredi Homera na timu yake kutumiwa ujumbe wa vitisho na maelekezo kutoka kwa 'watu wazito' kinyume cha yale ya Rais Samia na Baraza la Mawaziri.

> "Usiijaribu Serikali. Sasa tunajenga kilomita 350 za barabara kutenganisha hifadhi na vijiji. HOMERA"

Taarifa za ndani zilizolifikia gazeti hili zinadai kwamba kama si msimamo imara wa Homera na wasaidizi wake ambao pia walitishiwa hata kudhuriwa afya kwa njia za kishirikiana, ng'ombe hao wangerejeshwa kwa wafugaji wakorofi.

Alipoulizwa kuhusu 'vimemo' na maelekezo kutoka kwa 'wakubwa', Komredi Homera alicheka na hakutaka kuzungumzia mambo hayo.

Kuhusu ushirikina, anasema kwa utani: "Tukaambiwa eti tukifika hatutawaona ng'ombe wala Bonde la Usangu. Tukaenda. Nikawauliza makomredi wangu, vipi jamani, hamuoni au mnaona? Wakanijibu kuwa wanaona na kazi ikaendelea."

**Mpaka mrefu kuwekwa**

Katika hatua nyingine, Serikali Mkoa wa Mbeya pamoja na wadau kadhaa, sasa wanaweka mpaka mrefu unaotenganisha eneo la hifadhi na la umma kwa kujenga barabara.

Komredi Homera anasema mpaka huo utakuwa ni wa barabara yenye urefu wa kilomita 350.

"Hii inatoka Madibira kupitia Kapunga hadi Mlima Mbeya. Sasa baada ya hapo hakuna atakayeruhusiwa kuwa upande wa pili wa barabara (mpaka) ambako ni hifadhi.

"Watu wote watapaswa kuhama na wengine kwenda NARCO (ambako kuna maeneo yametengwa kwa ajili yao)," anasema.

**Ukame unavyotishia uhifadhi**

Wakati idadi ya wanyamapori ikiongezeka katika mfumo wa ikolojia ya Ruaha - Rungwa, hali si shwari ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Hii inatokana na Mto Ruaha Mkuu (ambao ndio uti wa mgongo na uhai wa hifadhi) unaopita katikati ya hifadhi kukumbwa na ukame wa kutisha unaosababishwa na uharibifu wa mazingira.

Mto huu wenye urefu wa kilomita 475 unaoanzia kwenye 'beseni' la Bonde la Usangu mkoani Mbeya na Ihefu, hutiririsha maji kwenda kufua umeme Ruaha, Kidatu kisha kupita Kilombero hadi Bwawa la Nyerere katika Mto Rufiji.

Baada ya Mbeya, Mto Ruaha Mkuu hupita Iringa, Dodoma, Morogoro, Pwani na kumwaga maji Bahari ya Hindi unakofahamika kama Mto Rufiji.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell ole Meing'ataki, ambaye ni Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha, anasema Mto Ruaha Mkuu ndio unaoifanya hifadhi kuwa ya kuvutia.

Nyakati za kiangazi, maelfu ya wanyama hukimbilia mtoni kupata maji, hivyo kukauka kwake ni hatari kwa utalii ni uhifadhi hasa mfumo wa ikolojia ya Ruaha - Rungwa.

"Hali ni ngumu. Uharibifu wa mazingira umefanya mto kukosa maji kwa miezi mitatu. Hautiririshi maji. Yapo madimbwi madogo madogo ambayo maji yake ndiyo yanayotumiwa na wanyama, lakini ni machafu na hayatoshi.

"Ukiyatazama maji hayo yamebadilika rangi. Si maji ya kawaida. Ni maji machafu sna. Baadhi ya wanyama wanaishi humo, wengine wanafia humohumo!

"Kwa ujumla si maji salama kwa uhai wa wanyama, lakini hawana namna kwani ndiyo maji yaliyopo," anasema Ole Meing'ataki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa Oktoba mwaka huu.

Anasema hata wanyama nao pia huhitaji maji safi ya kunywa.

Kilomita 164 kati ya 475 za Mto Ruaha Mkuu zimo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, huku Bonde la Usangu linalodaka maji kutoka milima ya Mbeya na Makete mkoani Njombe nalo pia likiwa ndani ya hifadhi.

Ni uvamizi wa shughuli za kibinadamu kwenye Bonde la Usangu ndicho chanzo cha matatizo ya uhifadhi.

"Hizi shughuli za kibinadamu, uharibifu kama ukataji miti, uchomaji mkaa, uingizaji mifugo kinyemela kwenye bonde hilo na maeneo mengine ya vyanzo vya maji zinaathiri uhifadhi na ndiyo sababu kubwa ya maji kukauka," anasema.

Tatizo jingine ni upanuzi wa kilimo holela katika Bonde la Usangu na Ihefu kinachochepusha maji kuelekea mashambani bila kujali kwamba maji hayo ndiyo yanayostawisha maliasili hifadhini na mabwawa ya kufua umeme.

"Tunashukuru serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha Bonde la Usangu na Ihefu yanaendelea kuhifadhiwa. Tunafahamu pia umuhimu wa uamuzi wa hivi karibuni kuwaondoa wavamizi," anasema akiahidi kushirikiana na akina Komredi Homera kufanikisha kazi hiyo kwa manufaa ya taifa bila kunyanyasa wananchi.